FEBRUARI, 2024

# WILAYA YA IKUNGI

JARIDA LA KILA MWEZI

**Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi**

**"Wanaume tunapigwa na wake zetu hatusemi tu" Dawati la jinsia chukueni hatua**

**Uk 06**



## *Katibu tawala aongozo zoezi la upandaji miti katika shule ya Msingi Kipumbwiko*

*uk 08*




**Na mwandishi wetu,**

Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi lakaa Kujadili na kupitisha Rasimu ya mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 zaidi ya Bilioni 39.1 kwa ajili ya shughuli za maendeleo wilaya ya Ikungi

Pia baraza limejadili Rasimu ya mpango wa Bajeti ya TARURA Bilioni 4.4 pamoja na Rasimu ya mpango wa bajeti ya RUWASA Bilioni 4.7 ambapo Baraza tukufu la Madiwani limeridhia kupitishwa kwa bajeti hizo tayari kwa kuanza utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo Wilayani hapa







Kushoto Mkuu wa Wilaya ya Ikungi Mhe Thomas Apson kulia Mkurugenzi mtendaji Ndg Justice Kijazi- wakizindua program jumuishi ya malezi



**Nq mwandishi wetu**

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi Mhe.Thomas Apson amezindua programu jumuishi ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (PJT-MMMAM-2021/22-2025/26) katika Wilaya ya Ikungi

Akizungumza kabla ya uzinduzi huo leo tarehe 07 Februari 2024 amesema uzinduzi huu kiwilaya ni mwendelezo wa kuimarisha utekelezaji wa program jumuishi ya taifa ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 13 Desemba, 2021 ili kutekeleza na kuleta matokeo chanya kwa Taifa letu

"Hii ni kielelezo cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan kujielekeza kwenye kuweka misingi imara zaidi ya malezi na makuzi ya watoto wa Taifa hili ili watoto waendelee kukuwa katika utimilifu wao kuanzia hatua za awali za ukuaji wao pia program hii inalenga kutoa afua stahiki kwa watoto wenye Ulemavu ili kuondoa au kupunguza athari za makali kwa watoto wenye Ulemavu na hivyo kuwa na fursa pana zaidi za kufika mbali katika kutoa mchango wao kwa taifa lao", amesema Mkuu wa Wilaya

Ndg Justice Kijazi ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi amesema kuwa vitendo vya Ukatili havikubaliki na ndio maana Sheria kali imekuwa ikichukua mkondo wake kwa wale wanaobainika kufanya vitendo hivi

"Hivyo ni jukumu letu kama viongozi kuchukua hatua panapotokea matendo ya kikatili hasa kwa watoto wadogo",amezungumza Mkurugenzi

Kwa upande wake Beatrice Maeda Afisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Ikungi ameongeza na kusema kuwa atashirikiana vyema na viongozi wa kata Vijiji na vitongoji kuhakikisha Elimu inafika kuepusha na kubaini vitendo viovu vinavyopeleka ukatili hasa Kwa watoto.



**Na mwandishi wetu**

Wabunge wa Majimbo ya Singida Mashariki na Magharibi Mhe Jumanne Miraji Mtaturu na Elibariki Kingu wamekabidhi magari mawili aina ya landcruser kwaajili ya huduma za haraka (Ambulance) katika hospitali ya Wilaya ya Ikungi na kituo cha afya Sepuka ili kurahisisha huduma za afya kwa wagonjwa walio zidiwa .

Wakizungumza katika makabidhiano hayo leo Tarehe 04 februari,2024 Mhe Mtaturu amesema kuwa serikali imetoa magari hayo katika wilaya ya Ikungi kwa madhumuni ya kuepusha vifo vitokanavyo na kucheleweshwa kwa wagonjwa pale wanapozidiwa .

"Zaidi ya milioni 140 zimetumika kununua gari mmoja hivyo serikali imeipa kipaumbele sekta ya afya kwa madhumuni pia ya kuepusha vifo vya mama na mtoto" amesema Mtaturu

Kwa upande wake kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi Bi Haika Massawe amesema kuwa wapo tayari kushirikiana na mganga mkuu na mganga mfawidhi kuhakikisha magari yanatunzwa na kutumiwa kwa malengo mahususi ya kubeba wagonjwa.

Baadhi ya wananchi walio hudhuria katika makabidhiano hayo wamesema kuwa wanamshukuru Raisi Wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwajali wananchi wa Ikungi kwa kuletwa kwa huduma hii ya Ambulance katika hospitali ya Wilaya. Mwisho Mhe Mtaturu ameomba gari lililokuwa likitumiwa mwanzo litumike katika kituo cha Afya cha Ntuntu kutokana na umbali wa kituo hicho kilipo.

**Na mwandishi wetu,**

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi Mhe Thomas Apson apokea maagizo ya serikali ya kampeni ya utoaji wa chanjo ya Surua na Rubella katika Wilaya ya Ikungi inayotarajiwa kufanyika Kuanzia tarehe 15 mpaka 18 ya mwezi huu. Hayo yamesemwa leo Tarehe 09 Januari 2024 katika ukumbi wa Halmashauri ambapo katika Kujadili utekelezaji wa maagizo ya serikali ya utoaji wa chanjo ya Surua na Rubella amesema kuwa magonjwa ya Surua na Rubella huenezwa kwa njia ya hewa hususani pale mgonjwa anapokohoa au kupiga chafya na maambukizi huwa ni ya haraka sana hasa sehemu zenye msongamano.

" Tunalo jukumu kama Wilaya kutoa chanjo hii mapema iwezekanavyo ili kuokoa watoto katika janga hili", amezungumza Mhe Apson Akisoma taarifa Afisa Afya Wilaya ya Ikungi Ndg Abiudi amesema Ofisi ya Rais TAMISEMI imeandaa kampeni shirikishi ya kitaifa ya utoaji wa chanjo ya Surua na Rubella ili kuweza kuwakinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Surua na Rubella kwa kuwapatia chanjo hiyo .

Afisa Afya ameongeza na kusema kuwa chanjo hiyo itatolewa kwa watoto wa umri wa miezi 9 hadi miezi 59 na jumla ya watoto 55929 wanatarajiwa kufikiwa ndani ya siku 4 katika maeneo yao kama Sokoni, katika ofisi za Serikali, shuleni hasa katika shule za awali na Vituo vyote vya kulelea watoto. "Jumla ya timu 80 zimeandaliwa timu hizo zimehusisha watumishi kutoka kwenye vituo vya utoaji wa huduma za chanjo ya kila siku na kila timu itakuwa na watoa huduma watatu ambao ni mchanjaji mmoja, mtunza takwimu mmoja, na mhudumu ngazi ya Jamii mmoja, pamoja na mhamasishaji.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi amezungumza na kusema kuwa watendaji wa kata na vijiji wanalo jukumu kuhakikisha zoezi hili linaenda sawa kwa kuhakikisha wanafanya uhamasishaji kwa wananchi ili kuhakikisha watoto wote wanapatiwa chanjo kwa wakati kutokana na ratiba ilivyo. Kupitia kikao hiki pia idara ya afya imewasilisha taarifa ya lishe, taarifa ya M-MMAMA, taarifa ya ICHF,pamoja na taarifa ya tamko la jiongeze tuwavushe salama na zote zilijadiliwa na kutoa maadhimia ambayo yanalenga kuimarisha Afya za watanzania hususani katika Wilaya ya Ikungi. Kikao hiki kimehudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Ikungi,kamati ya ulinzi na usalama,katibu



**Na mwandishi wetu,**

Katika muendelezo wa ziara ya Tarafa Kwa Tarafa Mkuu wa Wilaya Mhe.Thomas Apson,Mkurugenzi Ndg.Justice Kijazi pamoja na Wakuu wa divisheni na vitengo katika Wilaya ya Ikungi waendelea kusikiliza kero za watumishi pamoja na wananchi Tarafa ya Mungaa ambapo baadhi ya watumishi wameomba kuboreshwa Kwa miundombinu ya shule na nyumba za watumishi ili kuwezesha watumishi kuwa na Ari ya kufanya kazi katika mazingira rafiki.

Akizungumza katika kikao Cha ndani Mkurugenzi mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi amesema kuwa Moja ya mambo ambayo yamepewa kipaumbele katika mpango wa bajeti ya mwaka 2024/2025 ni pamoja na ujenzi wa miundombinu mashuleni na nyumba za watumishi ikiwa ni pamoja na vyoo, miundombinu ya maji pamoja na samani na vitendea kazi.

Sambamba na hilo Mkurugenzi ameahidi kutenga Milioni 50 katika bajeti ijayo kwa ajili ya kuhakikisha madawati yanakua sio tatizo katika shule zote Wilaya ya Ikungi

“Nitalisimamia hilo Kwa karibu kwani ni ahadi yangu kwenu lengo ni kumfanya mwanafunzi akae sehemu nzuri pindi anapofundishwa" amezungumza Mkurugenzi Kijazi

Katika kikao Cha nje ambacho kilihudhuriwa na Viongozi mbalimbali akiwemo Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe.Ally J.Mwanga, madiwani mbalimbali mwenyeji na kata za jirani

Mhe.Dc Thomas Apson wakati anajibu baadhi ya kero za wananchi amesema kuwa Kuna haja ya kupangwa kwa Tarafa ya Mungaa kwani imekua kwa kasi hivyo mji usipopangwa kunaweza pelekea migogoro mingi ya Ardhi

"Hata hivyo kutokana na ukuaji huo wa mji tunapaswa kujilinda na tatizo la magonjwa ya mlipuko kwani tayari Kuna wagonjwa kadhaa wa kipindupindu na watatu wamefariki, ujenzi wa vyoo bora ndio njia moja wapo ya kunusurika na ugonjwa huo kunawa mikono Kwa sabuni kabla ya kula na kuosha matunda" amesema Mkuu wa Wilaya ya Ikungi

Mhe Thomas Apson Pia Mkurugenzi amemuagiza Afisa Ardhi Wilaya ya Ikungi Bwana Salum kuwa kufikia juma tatu ya tarehe 26 mwezi wa pili 2024 yeye na timu yake wafike Tarafa ya Mungaa kutatua kero ya Mama aliyong'olewa bikoni za kiwanja chake na kupima maeneo ya wanaohitaji kupimiwa kwani miongoni mwa kero ambazo zimezungumzwa ni pamoja na maeneo kutokupimwa jambo linaloweza kupelekea migogoro ya Ardhi.

















*Maafisa kilimo wa Wilaya ya Ikungi hapo Jana tarehe 9 February ,2024 Ndg Msemo na Boniface wametembelea mashamba darasa ya Mahindi Mtama Alizeti na Viazi lishe katika kijiji cha Ntuntu,Kipumbuiko,Kituntu,Mahinmi,Nkunikana,Kideka,Unyahati,Ikungi,Kituntu ,Dung'unyi na Muungano*



**Na Mwanadishi wetu,**

## KILELE CHA UPANDAJI MITI WILAYA YA IKUNGI 2024

Katibu Tawala wa Wilaya ya Ikungi Ndg Rashid M.Rashid aongozo zoezi la upandaji miti katika shule ya Msingi Kipumbwiko akishirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi Ndg. Justice Kijazi kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi Mhe. Thomas Apson

Akisoma taarifa hiyo Bwana Legan Elfoni Afisa Misitu wilaya ya Ikungi amesema kuwa wilaya ya Ikungi inatarajia kupanda jumla ya miche 1,500,000 katika maeneo mbalimbali ambapo mpaka kufikia tarehe 14/02/2024 jumla ya miche ya miti 127,571 imesambazwa na kupandwa katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Ikungi na zoezi la usambazaji wa miche linaendelea

Ameongeza na kusema kuwa miche ya miti iliyosambazwa na kupandwa ni pamoja na miti ya matunda, mbao, na kivuli na leo katika zoezi hili miche ipatayo 1,000 katika maeneo ya umma, taasisi pamoja na maeneo ya watu binafsi itapandwa.



"tunapenda kukushukuru tena Mhe Mgeni Rasmi viongozi na wananchi wote mliofika katika maadhimisho haya ya kilele cha upandaji miti kwa msimu wa mwaka 2024 hivyo ni jukumu letu kwa ujumla kusimamia na kuitunza miti iliyopandwa kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho"amesema

Afisa Misitu. Kwa upande wake mgeni Rasmi katika zoezi hilo amesema mwamko wa upandaji miti katika wilaya yetu unazidi kuimarika mwaka hadi mwaka kutokana na wananchi kupata elimu ya kuhifadhi mazingira kwa njia ya kupanda miti ya aina mbalimbali kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yanayosababishwa na uharibifu wa mazingira.





"Nitoe rai kwa viongozi wote tuzidi kutoa elimu kwa wananchi na wanafunzi juu ya umuhimu wa upandaji miti na uhifadhi wa mazingira kwa mustakabali wa maisha yetu kwani miti ni uhai",amezunguza DAS

Aidha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi Ndg Justice Kijazi ametoa shukrani za dhati na kulipongeza Shirika lisilo la Kiserikali la Trees For The Future kwa mchango wao mkubwa waliotoa katika kufanikisha zoezi zima la kuandaa kitalu cha miche katika kijiji cha Mungaa ambapo sehemu kubwa ya miche inayopandwa msimu huu inatokana na kitalu hicho.

## Na mwandishi wetu

Waheshimiwa Madiwani wasisitiza Walimu kujengewa nyumba.

Katika kikao hicho cha kamati ya huduma za jamii hapo Jana 5 February,2024 waheshimiwa wamesisitiza walimu wajengewe nyumba za kuishi ili wawe karibu na mazingira ya shuleni kwani makazi ya watu maeneo mengi ni mbali kutoka shuleni lengo walimu wafundishe kwa wakati na kwa ufanisi zaidi.

Mhe Gabriel Dulle,Abel Nkuwi na Abel Suri wameomba shule za Mve ,Nali na Matongo zifanyiwe ukarabati wa haraka kwani ni shule kongwe zimekuwa chavu mno lengo kuepuka maafa haswa kipindi hiki cha mvua.

Pia Mhe Suri ameongeza kwa kusema kitengo cha TASAF kiangalie walengwa wenye sifa kweli wa kupewa pesa hizo na kutoa mafunzo kwa mikataba wanayowapa ili kupata uelewa zaidi.

Mhe Leornad Nkwae nae ameomba kwenye bajeti ya 2024/2025 awekewe bajeti walau ya chumba kimoja cha maabara cha shule ya Sekondari Iseke Muungano pamoja na kumaliziwa boma la shule mpya ikhoree lililojengwa na nguvu ya wananchi .

Mwisho Mwenyekiti wa kamati hiyo ya huduma za jamii Mhe Stephani Missai amesisitiza watoto waliofikia umri wa kwenda shule waende shule, wanafunzi waendelee kupata lishe mashuleni ili kuongeza ufaulu na wazazi wajitahidi kufuatila maendeleo ya watoto wao mashuleni.










**Na mwandishi wetu,**

Afisa Nyuki Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi bwana Philbert Benedict akishirikiana na wataalamu wengine watoa mafunzo juu ya mbinu za ufugaji Nyuki kibiashara katika kutekeleza mradi wenye jina "Kuwezesha ufugaji Nyuki katika vijiji kumi vinavyozunguka msitu wa Minyughe kwa uboreshaji wa kipato ili kupunguza uharibifu wa hifadhi ya msitu wa Minyughe uliopo Wilaya ya Ikungi mkoa wa Singida.

Mafunzo hayo yametolewa Kuanzia Tarehe 30 mpaka 31 Januari mwaka huu katika kijiji cha Mnyange na Iglansoni ambapo mafunzo hayo yanalenga kukuza mbinu za ufugaji Nyuki kibiashara na yametolewa kwa vikundi viwili vyenye jumla ya washiriki 60.

"Vikundi hivyo viwili ni kutoka Kata ya Iglansoni kwa maana ya Vijiji viwili ambavyo ni Iglansoni na Mnyange washiriki 30 kutoka katika kila kikundi na mafunzo yalifanyika kwa nyakati tofauti"amezungumza Afisa Nyuki

Afisa Nyuki ameongeza na kusema kuwa mradi huo unafadhiliwa na Mfuko wa misitu Tanzania (TaFF) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi. Sambamba na hilo Afisa Nyuki ametaja Vijiji hivyo kumi ambavyo vitafikiwa na mradi huo kuwa ni pamoja na Iglansoni, Mnyange, Ng'ongosoro, Muhintiri, Makilawa, Mtavira, Mtunduru, Germani, Mwaru na Mpugizi.

# HALMASHAURI YA WILAYAN YA IKUNGI

# JARIDA LA KILA MWEZI

## JARIDA LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA HABARI NA MAWASILIANO

## FEBRURI, 2024

*NAMBA:+255 682 404 347*

*KWA MAONI*